



East African Journal of Swahili Studies

ejss.eanso.org

Volume 8, Issue 1, 2025

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>



EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

Kutumiya Alama za Kifasihi Kisiyasa ili Kušajiiša Mṭaji wa Kijamii: Kad'iya ya Sufi Manalemba Kuvunja Upanga katika Uṭeṇḍi wa Siri Li Asrari

Mohamed Karama^{1*}, Arthur Muhia², Kineene wa Mutiso³ & Rocha Chimera⁴

¹Chuo Kikuu cha Kabianga, S. L. P. 2030 - 20200, Kericho, Kenya.

²Chuo Kikuu cha Pécs, 48-as tér 1, 7622 Hungary.

³Chuo Kikuu cha Nairobi, S. L. P. 30197-00100, GPO, Nairobi, Kenya.

⁴Chuo Kikuu cha Pwani, S. L. P. 195-80108, Kilifi - Kenya.

* Barua pepe ya mawasiliano: mkarama@kabianga.ac.ke

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2760>

Tarehe ya Uchapishaji: IKISIRI

12 Machi 2025

Istilahi Muhimu:

Siyasa,
Dini,
Sufi,
Manalemba,
Kutumiya Siyasa,
Kuleta Siyasa,
Mṭaji Kijamii

Fasiri nyengine za kazi za kifasihi zapatikana ka kutiliya maanani muktad'a wa kihistoriya wa kazi hiyo. Fauka ya hayo, itikaḍiza kisiyasa, kiḍini, au kijinsiya ni miyongoni ma paradimu zinazoongoza muwonoulimengu wa mtunzi wa kazi za kisanaa. Katika mfanyiko huu wa kučanganya masiyala ya kijamii na ya kiimani nripo uṭafiti wetu ulipoḍ'amiriya kuuhakiki Uṭeṇḍi wa Siri Li Asrari uliyotunga ni Manamarabu binti BanaLemba mnamo 1662 huko Pate, Kenya. Makala yetu yamejaribu kujibu maswali: muktad'a wa kihistoriya wa wakaṭi na mahali ulimšajiišaje mtunzi kuwasiliša d'amira yake ka mbinu ya kinahau? Je, ḍini, haswa d'ehebu la kiSufi, iličangiyaje muwonoulimengu wa mtunzi wakaṭi wa kuwasiliša alama za kiḍini katika kazi hiyo? Je, suluhišo la mtunzi kuhusu muktad'a wa siyasa ya wakaṭi huwo ka mkonro wa imani yake ulitatuwaje maafa ya wakaṭi huwo? Tuličanganuwa maṭini ya uṭeṇḍi huu tukiyoongozwa ni nad'ariya ya uHistoriya Mpya ka kangaziya: alama, jazanra, ṭaswira, siṭiyara, kiyasi zilivotumiwa na mtunzi na aṭ'ari zake katika mfanyiko mzima wa kisiyasa. Data ya upili ilikusanywa ili tupate fasiri nyenginezo kuṭokana na muktad'a huwo ka sababu hayakujitokeza mayelezo haya katika uṭeṇḍi. Maṭokeyo yetu yanad'ihiriša: ka kučanganuliwa luḡa ya nje kiyasi ya vita va Mtume Muhammad (mhusika nguli) na And'aruni (mhusika nruli) ilikuwa ni siṭiyara ya matukiyo ya wakaṭi huwo. Hali kad'alika, mtunzi ališajiišwa ni matukiyo hayo kenye uwasilišaji wake ambawo ulifasiri nahau za kusikiya siyasa (hisiya zake za muktad'a wa wakaṭi, mahali, na hali), kingiliya siyasa (kuyazungumziya matukiyo), na kuleta siyasa (kukosowa kupita mipaka)—unukud'i wa msimamo wa aila yake ambao ni sosiyasa (maSufi hawaingii siyasani). Kinyumeče, data ilipočanganuliwa ka minatarafu ya luḡa ya nrani ya kifasihi ya

kiSufi ilid'ihirika maana ya nahau kutumiya siyasa ni kutumiya hekima kuwaaid'i waumini wamtegemee Mungu tu ka matatuzi ya matatizo yote yanayowakabili hivo "kuvunja upanga" wa siyasa na kuweka imani ka Menyezi Mungu. Utafiti wetu una natija ya kuwafafanuliya wanaluga umuhimu wa nahau za kiSwahili katika fasihi na haswa ikiwa nahau hizo zina a'ari za uhasi kama lilivo neno siyasa leo.

APA CITATION

Karama, M., Muhia, A., wa Mutiso, K. & Chimera, R. (2025). Kutumiya Alama za Kifasihi Kisiyasa ili Kušajiiša Mtaji wa Kijamii: Kad'ia ya Sufi Manalemba Kuvunja Upanga katika Uteŋdi wa Siri Li Asrari. *East African Journal of Swahili Studies*, 8(1), 201-215. <https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2760>

CHICAGO CITATION

Karama, Mohamed, Arthur Muhia, Kineene wa Mutiso and Rocha Chimera. 2025. "Kutumiya Alama za Kifasihi Kisiyasa ili Kušajiiša Mtaji wa Kijamii: Kad'ia ya Sufi Manalemba Kuvunja Upanga katika Uteŋdi wa Siri Li Asrari". *East African Journal of Swahili Studies* 8 (1), 201-215. <https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2760>

HARVARD CITATION

Karama, M., Muhia, A., wa Mutiso, K. & Chimera, R. (2025) "Kutumiya Alama za Kifasihi Kisiyasa ili Kušajiiša Mtaji wa Kijamii: Kad'ia ya Sufi Manalemba Kuvunja Upanga katika Uteŋdi wa Siri Li Asrari", *East African Journal of Swahili Studies*, 8(1), pp. 201-215. doi: 10.37284/jammk.8.1.2760

IEEE CITATION

M., Karama, A., Muhia, K., wa Mutiso & R., Chimera "Kutumiya Alama za Kifasihi Kisiyasa ili Kušajiiša Mtaji wa Kijamii: Kad'ia ya Sufi Manalemba Kuvunja Upanga katika Uteŋdi wa Siri Li Asrari", *EJSS*, vol. 8, no. 1, pp. 201-215, Mar. 2025.

MLA CITATION

Karama, Mohamed, Arthur Muhia, Kineene wa Mutiso & Rocha Chimera. "Kutumiya Alama za Kifasihi Kisiyasa ili Kušajiiša Mtaji wa Kijamii: Kad'ia ya Sufi Manalemba Kuvunja Upanga katika Uteŋdi wa Siri Li Asrari". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 1, Mar. 2025, pp. 201-215, doi:10.37284/jammk.8.1.2760.

UTANGULIZI

Binaadamu ni kiyumbe wa siyasa, čembelečo Aristotle (*Politics I*). Siyasa haiyepukiki, imo nrani ya kila binaadamu, mume au mke. Mašujaa wanawake na wanaume wa Afrika wamešikana kupiganiya uhuru wa maAfrika na wanatambuliwa ka ušujaa wawo. Anapotajwa Mekatilili wa Menza (wa *Midzičenda*), Syokimau (wa *Kamba*), Mukami wa Kimat'i (wa *Gikuyu*) wanaŋi wa Kenya wanaona fahari na kujinasibiša na majagina hao kenye ulingo wa kisiyasa. Ka waSwahili hali kad'alika, Manakupona binti Mšamu, Mamake Fumo Liyongo, na kijakazi Saada wamešerehešwa kama wakombozi wa wana wawo (Biersteker, 1991). Makala haya yanamangaziya šujaa Manamarabu binti Banalemba (ajulikana kiufupi, ManaLemba), manamke aloiši katika Karne 17 uSwahilini, alotumiya kalamu yake na ubingwa wa ušairi kupinga ud'alimu wa kiPortuges uliyotawala kimabavu Afrika Mašariki ka miyaka miya mbili

(1498—1729); čembelečo Pannikar (1953) akinukuliwa na Sheriff (2002, uk. 15) uwanzilizi wa kipinri ča kihistoriya ča Vasco da Gama katika Bahari Hindi.

ManaLemba, mtunzi wa *Uteŋdi wa Siri li Asrari* (soma *Siri*), alizawa katika familiya ya wasomi wa kiIslam na babake alikuwa šekhe mkuu katika taifa-jiji la Pače. Familiya hii yajulikana ka jina Jamalullayli iliyotoka Had'ramuŋi, Yemen katika Karne ya 16 na kuseleleya Pače (Bang, 2003, uk. 25). Pače wakaŋi huwo ni mji na dola tukufu uSwahilini ikijulikana mpaka bara Arabu. Kiličowahamiša kutoka kawo Had'ramuŋi na kuja huku ni matatizo mengi yalowakumba, mojawapo ni mašambulizi ya maharamiya walovamiya miji yawo kila mara (Bang, 2003, uk. 23). Manziliši wa BaAlawy, *tariqa* ya kiSufi, Al Faqih Al Muqaddam Muhammad bin Ali mnamo Karne ya 13 huko Had'ramuŋi (Bang, 2003, uk. 13), ališika msimamo wa amani na kabuđu Mungu tu bila ya kujiingiza

kenye siyasa za aina yoyote; hatuwa hii ikijulikana “kuvunja upanga” (Bang khj; Rumman, 2020, uk. 280). Hii ni ka sababu uSufi uliçipuka, kulingana na Ibn Khaldun, baada ya mazingira ya kiIslam ulimenguni kuwanza kenra kinyume na Qurani na mafundišo ya Mtume Muhammad, misingi miwili ya itikaçi inayotegemewa na waIslam wote (Muhammad, 2003, uk. 28). Mašekhe wa wakati huwo wakaoneleza kujitowa kanro na kufuwata njiya ya kujisafiša mili, moyo, na imani ili kupata uwongofu na kepuka maçafu ya nafusi. Ka mintarafu ya mrengo huu, ıauliza: je, çini, haswa d’ehebu la kiSufi, iliçangiyaje muwonoulimengu wa mtunzi wakati wa kuwasiliša fikira za kiçini katika kazi hiyo?

Siyasa ni neno la kiArabu ambalo usuli wake ni neno “[a]sasa” lenye maana ya “mzizi wa k^{hithu} au jambo” na katika masiyala ya kijamii lina maana ya “uwongozi na utawala wa wat^{hu}” (Mustafa, 2004). Kulingana na David Easton (1979, 1981) akinukuliwa na Heywood (2013, uk. 4) anasema siyasa ni upaji wa rasilimali kutokana na mamlaka alonayo mtawala alohalališwa ni jamii. Siyasa piya ni namna ya kusuluhiša mitafaruku ka kukaa pamoja na kuçauriyana na kukubaliyana bila matumizi ya nguvu. Rom (2022, uk. 8) na Heywood (2013, uk. 2) wanayezeza kuwa siyasa imekuja kunasibišwa na ujanja au urongo hivo kulipa neno na sifa ya atari mbaya. Aid’an, tukirejeleza matumiyaji ya neno hili “siyasa” kinahau kiSwahili, tutakuta siyasa huweza kumaaniša ‘ujanja’ katika msemu “kufanya siyasa” na huweza kumaaniša ‘hekima’ (Madan, 1903); yenye atari nzuri, katika msemu “kutumiya siyasa”. Maana zothe mbili katika utendi huu zimewasilišwa. Ikizingatiwa maana ya siyasa, ıauliza: muktaða wa kihistoriya na kisiyasa, wa wakati na mahali, ulimşajiişaje mtunzi kuwasiliša d’amira yake ka mbinu ya kiyalama?

Japo msimamo wa kiSufi ni wa amani usojiingiza kenye siyasa, Bujra (2017, uk. 228) anayezeza kamba pana haja ya tfafiti ziçunguze namna gani maHadrami (ManaLemba akiwa mmoja wao) walivotekeleza jukumu lao la kisiyasa, kiyuçu, na

kiyuçamaçuni katika maçaifa-jiji ya eneo hili la ustaarabu wa kiIslam wa waSwahili, Afrika Maşariki. Fauka ya hayo, mayelezo ya uSufi hayana buçi kutiliya maanani luça ya waşairi wa kiSufi ambayo ilikuwa tafauti kuliko luça ya kawaida—haça ya kiçini ya kiIslam—ka sababu ilieleza mahusiyano ya kiungu ambayo mara nyingi hayaelezeki na hayaeleweki (Wilde, h.t., uk. 2), kutokana na ubinafsi wa tajariba ya wanaopatana na tukiyo hilo la upeo wa tajariba (Bang, 2003, uk. 32; Schimmel, 1975, uk. 13). Mbali ya muktaða wa kihistoriya, kiçini (kiSufi), kuna na luça ya kimaçumbo na kiyalama ambayo huifanya luça ya kiSufi kuwa nzitho na ngumu keleweka hivo kuhiçajiya kubainiřwa katika siri zilizofiçamana nranime (Tindall, 1955, uk. 7; Rumman, 2020, uk. 27, 36; Abou-Bakr, 1992, uk. 23); na haça wakiyaeleza watakoseya katika mayelezo ka sababu ni kupita upeo wa fikira razini za manadamu (Al-Ghazali, 1952, uk. 55). Kama alivomsahihiša Mtume Muhammad Sayyidna Abubakar alipoota kuwa Mtume amemita na ilhali Mtume hakumita (beti 80—417).

Tukiyliza: je, suluhišo la mtunzi kutokana na muktaða wa siyasa ya wakati huwo ka mkonro wa imani yake ulitatuwaje maafu ya wakati huwo? Mapitiyo yetu kuhusu *Siri* yanabainiřa utendi huu imma umetajwa tu—Mulokozi na Sengo (2005) waliyuçaja tu kenye orod’a yawo ya tñendi za kiSwahili za kabla ya karne ya 20; umeelezwa sehemu fulani ka natari—Knappert (1979) aliyañdika ploti au sehemu ya vita tu ya utendi ka luça ya natari; ulipata kutafsiriwa ka kiJarumani (Dammann (1940) na ka kiIngeresa wa Mutiso (2003); au uliřugulikiwa katika sehemu za kiçini bila kufungamaniřa siyasa au uřiriki kenye siyasa (Karama, 2018; Karama, Chimerah, & wa Mutiso, 2018 & 2021). Katika kazi zothe tulizokiřataja awali: mosi, hakuna haça moja ilouweka utendi huu katika muktaða wa mandari alokuwamo nrani yake mtunzi—wakati wa utawala wa Portugezi kenye Paa za Afrika Maşariki mnamo Karne 15—17. Pili, masiyala ya siyasa, utawali na matukiyo yaloçokeya

wakaṭi huwo pamoja na kujiingiza mtunzi katika siyasa hiyo waṭanganuzi tulowataja hawakuyaṣuḡulikiya masiyala haya. Tḥatu, ijapokuwa Karama (2018) anayeleva kuhusu mukṭad'a wa kiSufi ambawo ulimaṭ'iri mtunzi na anawakifiṣa d'amira kuwa mategemezi ya ḡini nriyo suluhiṣo la matatizo ya manaḡamu. Jawabu la swali hilo ni: fasiri ya kamba mtunzi alipoṭeuwa kutumiya siyasa—kihekima—kenye ḡini kuwa nrilo *suluhuṣo pekee* la matatizo haṭa ya kisiyasa, halikujiṭokeza katika uṭanganuzi huwo na ṭanganuzi zoṭḥe zilotanguliya.

MSINGI WA NAḡARIYA

Msingi wa naḡariya tuṭakawotumiya ni ule unawopenḡekezwa ni naḡariya ya kifasihi ya uHistoriya Mpya. Mhimili mkuu wa naḡariya hii ni kamba matukiyo ya kihistoriya yana mṭango katika kazi za kifasihi, hivo basi, matukiyo hayo yanaweza kupawa fasiri zaiḡi kuṭokana na mukṭad'a wa mahali na wakaṭi wa matukiyo hayo (Bertens, 2001). Pili, wahakiki wabainiṣe migongano na miṭafaruku ya kijamii inayojiṭokeza katika kazi hizo. Migogoro hii husababiṣa mivutano ya fikira mbalimbali zinazopiganiya kuṭokuwa uwongozi wa fikira yenye nguvu. Hivo basi, kangaliwa ka kazi za kifasihi kihistoriya kutizame kenye uṣinrani huwo wa kinguvu na ṭena ka upekee wa kazi hiyo. Ni lazima kazi hiyo iyangaliwe kiyupekee ka sababu jambo lililosababiṣa maṭokeyo ya matenro hayo katika historiya ya maṇḡiṣi yaliṭokana na mahali na wakaṭi maalumu katika muḡa wa kuwako jamii hiyo. Ka miṇṭarafu ya ufafanuzi huu wa naḡariya ya uHistoriya Mpya, makala haya yaṭauṭanganuwa uṭeṇḡi wa *Siri* ka kangaziya mukṭad'a wa kimahali, kihistoriya, na kihali (kiḡini) zilizosababiṣa mtunzi kuwasiliṣa maud'uwi na mbinu za uwaṇḡiṣi alotumiya kufikiṣa d'amira yake kuu. Ka kutumiya fasiri za kinahau za neno “siyasa” nrivo tuṭakavod'ihiṣa masimulizi kuhusu matukiyo ya kihistoriya yalomfanya mtunzi kiṭaṭ'mini na hiṭimiṣoni kupenḡekezwa suluhiṣo lake la matatizo yalokabili jamii yake. Iṭakuja kuḡihirika kuwa kila kipanre ṭa simulizi kina “iṭikaḡi ṭeule” inayoifanya

kila iṭikaḡi ya kifikira kuṭowa suluhiṣo la tatizo lililokabili haṭimaye iṭikaḡi yenye nguvu nriyo mṭawala na kuzifanya iṭikaḡi nyenginezo mṭawaliwa. Nriposana, ManaLemba akapenḡekezwa, na akiyamini, iṭikaḡi ya kiḡini ya kumpekeṣa na kumṭawaliṣa Mungu katika majambo yoṭḥe nripo uṣinri d'iḡi ya matatizo yoṭḥe uṭapatikana.

MBINU ZA UṬAFIṬI

Uṭafiṭi wetu ulikuwa wa uṭanganuzi-maṭini wa *Siri*, nakala ya Dammann (1940) yenye beṭi 563. Tulikusanya data ya msingi kuṭoka vifungu va maneno venye d'ana ya kivita, kiḡini, kikawaiḡa, kiyalama, kisiṭiyara, kijazanra, na kiṭaswira vinavokamiliṣa maud'uwi na mbinu za uwaṇḡiṣi alotumiya mtunzi kufikiliza d'amira yake. Hali kad'alika, tulikusanya data ya upili na kuuweka uṭeṇḡi huu kenye mukṭad'a wa kimahali, kiwakaṭi, na kihali ili tufahamu yaliyosababiṣa matukiyo na matumiyaji ya vifungu va maneno hayo. Ka kufanya hivo (kuṣirikiṣa mukṭad'a) tulikiḡi mahiṭaji ya mihimili ya naḡariya ya uHistoriya Mpya. Mbali ya kuṭafiṭi mukṭad'a wa kihistoriya, piya tuliyakisi d'ana zilizomo uṭeṇḡini za “kuṣiriki kenye siyasa”, “kumpekeṣa Mungu”, na “kuṣajiiṣa” katika ṭasniya nyenginezo kama Sayansi ya Siyasa, uSufi, na Soṣolojiya kimṭawaliya, ili kufafanua kiṭimilifu maana za d'ana hizi na zinavowezeṣa uṭanganuzi wa uṭeṇḡi huu ka mkabala wa d'ana hizi.

MATŌKEYO

Kenye sehemu hii tuṭaangaziya namna ManaLemba alivoaṭ'iriwa na usuli wa na iṭikaḡi ya familiya na jamii yake haṭa akawa sosiyasa au menye siyasa. Je, siyasa ya ManaLemba ni ipi?

ManaLemba sosiyasa

Sell (2023, uk. 185) anafafanua sosiyasa ni kuṭojiṣuḡuliṣa au kuṭoṣiriki kenye siyasa; kuṭojitiya kenye mrengo wowoṭḥe wa kisiyasa. Ni manajamii kuṭojihusiṣa katika masiyala yanayoṭ'iri jumuiya ingawa ana ufahamu na ana uwezo wa kufanya hivo (Roskin, 2012, kur. 119-122). Haya mara

nyingi huotokea wakati mthu hawoni faida ya kujiingiza ka sababu hata akijiingiza katika kusema hakuna tafauti yoyote itakayotokea. Aina hii ya kuširiki kenye siyasa huweza kutokea ka sababu ya makuzi ya kisiyasa katika familia nyumbani au wat^hu wa karibu katika jumuiya. MaSufi wanajulikana kuwa wawo ni sosiyasa kabisa (Rumman, 2020, uk. 351; Hanieh, 2011, uk. 185) lakini ni Bang (2003, uk. 16) nriye anayeweka wazi kuwa BaAlawy (pote la kina ManaLemba) hawakujiingiza kenye siyasa kabisa wala hawakubeba silaha wakati wali(na)poiši baina ya wanajamii wengine, nriposana mitifaki mkuu wa *tariqa* (njiya) hii Al Faqih Al Muqaddam “alivunja upanga” kama alama ya kutojijusiša kabisa kenye vita wala siyasa baada ya katiriwa na uSufi. Jukumu lawo limekuwa keneza dini ka njiya ya kuwaaidi wat^hu kuhusu šariya na miyeneno ya Mtume Muhammad tu na kuwavutiya wat^hu wengine kenye dini ya kiIslam na kutangamana na wenye dini nyenginezo ka wema bila kuleta migongano baina ya wanajamii (Rumman, 2020, uk. 351). Walakini, čembelečo wa Thiong’o (1994, uk. 73) manajamii hawezi kupuka siyasa ka sababu mara hujikuta yumo siyasani bila ya kudamiriya kama Bang (2003, uk. 34) anavotubainiŝiya kuwa jina la mthu na kizazi čake huweza kuwa iŝara ya nguvu (siyasa) zilizomo kenye utajo huwo.

Mtunzi wa *Siri* aiŝa “Manamarabu” binti Ahmad “BanaLemba” bin Harun “Menye Hassan” bin Abd al Rahman bin Ahmad bin Abdallah bin Muhammad “Jamal al Layl” (ngamiya wa usiku au menye kukeša akimabuđu Mungu) (Sameja, uk. 244). Čenra kizazi hiči hađi kumfikiya manziliŝi wa *tariqa* ya BaAlawy, Muhammad bin Ali akijulikana piya ka jina Al Faqih Al Muqaddam. Harun bin Abd al Rahman, pamoja na manawe Ahmad, nriye aliyegura kutoka Hadramuđi kuja Pate katika Karne ya 16. Ahmad akaowa hapo Pate na kujaaliwa kijana Abdallah “Sahib al Tuyur” (menye nrege/nyuni wengi) ambaye (Abdallah) baadaye aligura na wanawe Aqil, Ali, na Ahmad, kenra Ngazija K 17 miŝoni (Bang, 2003, uk. 25&26).

Hakika tulonayo ni kamba mtunzi menyewe aliweka saina yake katika utendi (beti 556—558) kamba yeye ni Manamarabu binti BanaLemba na babake alikuwa šekhe mkuba hapo Pate, Kenya. Mtunzi anasema:

556. *Na mkitaka nasabu
Isimu yangu na abu
Ni mimi Manamarabu
Na baba ina liwazi.*

557. *Baba wangu watapamba
Ita šekhe Bana Lemba
Ya Rabi alimuumba
Na majaza kamjazi.*

558. *Elimu na Kuruani
Alimjazi Manani
Naliŝanrwa Kivuđoni
Ka nruze na ka wazazi.*

Katika beti hizo mtunzi wa utendi anayeleva nasaba yake: babake ni BanaLemba na yeye menyewe aiŝa Manamarabu. Kawo ni Kivuđoni nriko ka mamama zake na maŝangazile. Ustađ Muhammad Šariff Said al-Beid’ amemtaja huyu Ahmad alikuwa akijulikana piya “Menye malemba” (Al-Beidh, 2011, uk. 2). Kamba “malemba” ni lakabu ya Ahmad piya imetajwa na Dammann (1940, uk. 274). Kifasihi, mtunzi yoyote, wa mašairi, riwaya, tamiliya, huweza kuweka saina kazi hiyo ili kuwoneša ilitungwa ni nani. Uhakika huu huwa wa nguvu katika mawađa ya uwađiŝi wa kidini na haswa ka mašekhe wa kidini ya kiIslam kuna isnađi “silisili” ya kizazi, imma ya familia au ya walimu walowasomeša. Hii silisili ya kizazi ni muhimu sana ka mašekhe, na hata wat^hu wa kawaiđa, ka sababu hufuwata mkonro hađi kufikiya ka Mtume Muhammad na huhifađiwa, ka mfano Jamalullayl wamehifađi kizazi čawo čote katika šajara lawo huko Hadramuđi (Bin Sumeyt akinukuliwa na Walker, 2017, uk. 176). Ka kizazi ča kifamilia ni kamba ukoo wawo wenra mpaka wafikiya mababu zawo Ahli Bayti na Mtume Muhammad. Ama kiyusomi wa kiSufi, kizazi hiči huruđi nyuma hađi kumfikiya Mtume Muhammad

ambaye nriye mlimu mkuu wa waumini wote wa kiislamu, na kurudiya nyuma ka Mlimu Jiburili na kuhitimika ka Mene Elimu zote, Allah Muumba (Bang, 2003, uk. 14). Hii nriyo nguvu ya nasabu kufika ka Mungu Menyewe.

Jambo moja linalojitokeza katika maelezo ya hapo juu ni majina ya watu waliyotajwa kuweka kenye madonroo (""") ka sababu humaaniša siyo majina yawo haswa, pengine. Au, yawezekana ilikuwa ni mtinro wa kita majina wakaŋi huwo katika mji wa Pate. Mfalme wa kanza wa Pate, Muhammad V, alikuwa akijulikana kama "Bana Gogo" alotawala mnamo 1565—1593 (Knappert, 1988, uk. 21). Au, pana kisa kilotokeya nriyo mtu menyewe akapawa jina hilo, ka mfano, "Jamal al Layl" na siku hizi "Jamalullayl" ŋekhe huyu kazi yake usiku alikuwa akitiya maji misikiti yote (Bang, 2003, uk. 25), au fasiri nyengine, alikuwa akikeŋa usiku kumabuŋu Allah (Sameja, h.t, uk. 244). Ama kuhusu "Bana Lemba" kuna maelezo mawili: mosi, ni mtu alikuwa akivaa kilemba (kivazi ŋa kiŋwani) (Bang, 2003, uk. 176); pili, manafunzi wa uSufi hufinika kiŋambara (*khirqā*) au huviŋwa kilemba maalumu ŋa ŋekhe mkuu wa kiSufi kama alama ya ŋeyo aliŋopata baada ya kufikiya ŋaraja ya juu ya uwanaŋuwoni wa kiSufi (Bang, 2003, kur. 110 & 188). Ama kuhusu jina la mtunzi wa Siri sisi kuliweka kenye madonroo na ŋapendekeza kuwa hilo ni jina-fiŋe ili asijulikane mtunzi ni nani ni kuŋokana na: mosi, kifasihi, alitumiya jina hilo ka sababu yeye ni manamke na wanawake wakaŋi wake (K 17) katika miji ya uSwahilini hawakukubaliwa "kujiŋowa nje" wakaonekana kenye mayeneo ya wanaume ka mfano uŋairini, au pengine ni kama alivofanya George Eliot (jina la kiyume la uwaŋdiŋi lakini menyewe ni manamke (Mary Anne Evans [Wikipedia.org])). Pili, muktaŋa wa wakaŋi wa matukiyo alokuwamo nrani yake—wakaŋi wa uŋawala wa kiŋalimu wa maPortugeŋi K16 haŋi K17—haukuruhusu yeye kujitokeza ka kuhofiya maŋokeyo yaŋakayomŋuru yeye au mzazi wake moja ka moja. Thatu, kama ŋaŋturi ya wakaŋi wake, watu hujulikana ka lakabu naye alitumiya lakabu

hiyo. Au, nne, mtunzi alikuwa haŋaki kujulikana jina lake halisi ka sababu ni haiba na ŋabiya ya maSufi hawapendi umaarufu, ka unyenyekevu wawo, huŋeleza kuŋuriwa na uŋajo ule mbele ya wanaŋamu na hivo kuŋukuwa pahala pa Menezi Mungu. Walakini, katika Siri mtunzi aliweza kipokonya aila yake ubora ka kuwaŋaja familiya bora zaidi ya Ahlul Bayŋi (Wenye Nyumba ŋukufu) ambawo ni Mtume Muhammad na mkewe Ali bin Abi ŋalib, manawe wa kike Bibi Faŋma, na wajukuu zake Hassan na Hussein ambawo Mtume Muhammad menyewe amesema waislamu wawapende watu wa nyumba yake ka sababu ya uŋa Mungu wawo na kujiŋtoleza kawo kenreleza ŋini ya Mungu (ubeŋi wa 15-16). Haŋa hivo, maSufi baŋo wanayengeza ka kufuwata aya kuwa "mtu bora ni mŋa Mungu zaidi" (Al Hujurat:13).

Ili kumtambuliŋa mbora wa watu ni nani, siyasa ya maSufi ni kamba walimŋtegemeya Mtume Muhammad kuwa kiyongozi wawo katika mambo yawo yote na nriyo wakaanziŋa "iŋikaŋi" ya *Haqiqa Muhammadiya* ambayo ilihusu ufungamaniŋo wa ŋariya ya kiislamu, njiya ya kufikiya upeo wa Ukeli, ambaye ka maSufi, ni Mtume Muhammad (Schimmel, 1975, uk. 227; Bang, 2003, uk. 18; Gulen, 2011, kur. xix—xx). ŋegemezi lawo lilikuwa Mtume Muhammad maŋadamu nriye kiyongozi basi awaongoza kenye sahali ya mambo haŋa yakiwa mambo yale ni mazito au yana haŋari au aŋawaombeya ka Mungu wafanikiwe. Nriyo maana mtunzi alimta Mtume Muhammad ka majina kaŋaa yenye kumpa ŋaraja ya juu kuliko wahuŋika wengine. Ka mfano, alimta "nrombezi/muwombezi", "kipendi" ka sababu ya ŋeyo aliŋopawa ni Mungu Menyewe "Mene kumŋi Mtume basi amemŋi Mungu" (AnNisa:80). Ikawa ŋahaŋa ya muumini haikamiliki ila lazima aŋajwe Allah iyaŋdamane na Mtume Muhammad.

Kusikiya siyasa (kumuktaŋiŋa kihistoriya)

Kiluŋa kusikiya ni mawimbi ya sauti yanayopitiya kenye vifaa va masikizi ya binaŋadamu na hapo kung'amuwa ujumbe kupitiya vifaa hivo. Ikitumika

kinahau “kusikiya” humaniša “kuhisi” ka mfano katika msemu “kusikiya njaa/raha/usingizi” ambayo kimantiki humaniša kuhisi njaa/raha/usingizi ambazo ni d’ana d’ahanifu. Kuwona piya hutumika ka maana ya kuhisi ka mfano kuwona raha/njaa. Ka minajili hiyo, sehemu hii itaud’ihirisha muktad’a wa mtunzi kanda aloyaandika kutokana na hisiya yake juu ya matukiyo muhimu yaliyoenreleya wakati wake na mjini mawo.

Tarehe ya kanda ka utendi huu nriyo itibati muhimu tuloweza kitumiya kukisiya kipinri alioishi mtunzi. *Siri* iliyandika 1074 BH/1662 BK kama ilivotajwa kenye ubeti 561—562. Tukitumiya tarehe ya 1662 BK tutaona huu ulikuwa wakaribiya mišo wa utawala wa mPortugesi katika upa wa Afrika Mashariki. MPortugesi alitawala ka nguvu na ukatili mkubwa upa huu tangu 1500 hadi 1729 ili kutiwa mkononi biyashara ya Bahari Hindi na piya keneza dini ya kiKristo (Sheriff, 2002, uk. 15). Mbali ya tarehe hiyo, Mulokozi na Sengo (2005, uk. 63) walidaniša nad’ariya tete ya waandishi wa mashairi wa zamani na kukuta idadi kubwa yawo (30% ya wasairi wasailiwa) ni wenye umri kati ya miyaka 41—60. Kutokana na takimu hii taweza kusema kuwa ManaLemba alizawa 1600 na kuishi hadi 1700 ikiwa tutačkuwa kiwango cha umri wa juu (1662 – 60=1602). Lakini ka sababu babake aliguriya Pate 1500—1580 labda miyaka 30 baadaye alizawa ManaLemba ka hivo aliishi 1610—1710. Tutaona tarehe zote mbili 1600/1610 zamfanya ManaLemba kuwamo nrani ya himaya ya Portugesi na aliyuwona ud’alimu walokuwa wakiufanya kawo Pate au alipata habari za ukatili huwo katika miji mingine ya uSwahilini kutoka Barawa, Mambasa, Pemba, hadi Kilwa.

Vasco da Gama aliwasili huku Afrika Mashariki 1498 na mara moja kuweka kambi za kiPortugesi ka nguvu ili kutawala biyashara ya Bahari Hindi iliyošamiri sana wakati huwo. WaSwahili nawo piya walishiriki kenye biyashara hiyo ka karne nyingi kabla kuja mPortugesi (Shariff, 1988, uk. 3). Ka sababu ya kupinga uvamizi wa kimabavu wa

mPortugesi kuteka biyashara hiyo, waSwahili na wenyeji wengine, ka mfano, waArabu, waHindi walidinra na hapo kanziša miyaka miya mbili ya “umagikaji damu usonekana katika histori ya upa huu” (Shariff, 1988, uk. 4). Miji mikubwa ya kibiashara wakati huu ilinyafurwa mali: d’ahabu, masuwa, pembe, ambari, ng’ombe, vakula (Shariff, 1988, uk. 3) isokadirika, kabla ya kubomolewa na kuteketezwa kabisa, ka mfano, Ungwana 1506 (Knappert, 1988, uk. 7, Martin na Martin, 1973, uk. 5); Mambasa 1505, 1528, 1587; Barawa 1541, Faza 1587 (Boxer & Azevedo, 1960, kur. 21—2). Wafalume wa mataifa-jiji (Faza, Lamu) haya waličinjwa had’arani na vičwa vawo kupeleka ugaibuni (Goa) kama itibati ya kuuliwa kawo (Boxer & Azevedo, 1960, uk. 24). Mad’ila haya yaliziidi mpaka kufikiya hadi wanajeshi, ka gogi lawo, hawakutaka kujipikiya makambini mawo bali waliingiya mijini na kuvamiya mekoni wanyakuwe čakula, ka mfano huko Pemba (Boxer & Azevedo, 1960, uk. 32). Čembelečo Boxer na Azevedo (1960, uk. 45) matukiyo haya mabaya hayakongopewa ni wananči wa miji hii bali ni mayelezo ya watumiši wa Serikali ya Portugesi waliyotuma kuja kučunguza na kušuhudiya ukhabiti huu na mayelezo yawo yakawafiki simulizi za wenyeji. Bali zaidi, miyaka miya mbili baada ya konroka mamlakani visa hivi va Portugesi bado vakumbuka ni wananči wa sehemu hizi.

Ikumbuke kamba mPortugesi Vasco da Gama alipokuja upa huu hakupokelewa vizuri ni wananči wa janibu hizi za Afrika Mashariki. Lakini histori ya inatambiya kuwa Sultani wa Malinri alimpokeya na kumanraliya safari ya kumpeleka India ka usaidizi wa nahod’a wa Malinri (Sheriff, 2002, uk. 16). Pili, mitafaruku baina ya mataifa-jiji haya ya uSwahilini yalimpa fursa mPortugesi aungane na wanamiji mad’aifu na vibaraka wake kuwavamiya wanamiji mengine (Boxer & Azevedo, 1960, uk. 16). Isitoše, matajiri waSwahili walijitoleya takriban askari 1500 wakiširikiyana na mPortugesi ili kihami Fort Jesus Mambasa wakati wa kuzingirwa kake (Sheriff, 2002, uk. 17). Iyeleweke hata hivo, kuwa

mataifa mengine ya ugaibuni yalijiingiza kenye vita hivi, ka mfano, maOmani na maTurkiya, ili kuteteya maslahi yawo ya kibiyašara (Sheriff, 2002, uk. 17). Mnamo 1689 Pate ilitawaliwa ni Oman, na Mambasa, baadaye iliingiya kenye himaya ya Oman piya.

Itad'hirika wazi kuwa ManaLemba akiwa msomi (rejeleza Karama, n.we, (2021)) aliyasikiya kama habari haya matukiyo, aliyačanganuwa, akayaakisi, na kuhiṭimiša juu ya mad'ila waliyokutišwa ni waṭawala maPortuges. Wananč'i wa kawo Pate waliyaḍ'ibiwa na wafalume kučinjwa haḍ'arani mbali ya uporaji na uteketezaji wa majumba yawo. La šani zaidi, kama tulivotaja awali, ni wanaješi kuvamiya mekoni majumbani na kuta vakula juu ya majiko bila kujali sitara ya wanawake kama yeye ManaLemba! Kisiyo letu ni kamba, ManaLemba, piya aliyačanganuwa matukiyo haya kuwili: yalimfaidi nani na wananč'i wa Pate wanabakišwa nini katika miliki yao. Ikiwa koṭhe kuwili hakukuwafaidi sasa wamrudiliye nani aweze kuwaokowa na wenye tamaa hizi za mali ya kilimengu? MaPortuges wanawapiga šadiḍi na wanawokuja kuwasaiḍiya wanačukuwa kiličobaki čembelečo waSwahili hunena, “asezečo mivi mganga ataye”. Nriyo hisiya ya ManaLemba kuhusu matukiyo haya yanayomfanya aingiliye siyasa. Tuṭaona kuwa ni ile hisi anayosikiya ManaLemba inamfanya ayeleze maoni yake kama wanavohiṭimiša Mulokozi na Sengo (2005, uk. 70) kuwa matukiyo ya kijamii hayawezi kumkepa mtunzi wowoṭhe wa mašairi, sawiya na mhimili wa naḍ'ariya yetu ya uHistoriya Mpya, labda awe ana mapungufu ya welevu au ni barakala; na ManaLemba hakuwa na yoṭhe mawili kama tuṭakavoeleza punre.

Kingiliya siyasa (kušajiika na kuširikišwa)

Kingiya ni kitenro ča kufanya kuwamo nrani ya k^hit^hu ili nawe ujumuike. Kinahau kingiliya jambo ni kujitosa na kuširiki kenye jambo hilo kikamilifu. Ka hivo, ManaLemba kingiliya siyasa ina maana ya kamba alijitosa kenye ulingo wa siyasa baada ya

kušajiika kuṭokana na matukiyo ya wakaṭi na mahali alipokuwako. Telewe manajamii kuširiki kenye siyasa ni jambo lisohiṭaji kutezwa nguvu au kušawišwa bali ni hiyari ya wanaṭhi kusimama na kusema ambayo yahitajiya kurekebišwa. Van Deth (2021) anafafanuwa kuwa uširikišwaji huu upanuliwe maana ili kila tenro ambalo liṭakuwa na čembe za kusema k^hit^hu ka faida ya jamii bila kušurutišwa ni kuširiki siyasani; ni kusimama na kusema juu ya jambo linavoenrešwa na wapelekaji mambo katika nčhi, miji, au maširika. Ka kufanya hivo mananč'i anakuwa manamaoni (Rom, n.we, 2022, uk. 158). Tufahamu kuwa ManaLemba aliyafanya haya ya kingiliya siyasa uṭeṇḍini katika sehemu ya “manzo” ya uṭeṇḍi (beti 32—363).

Sehemu ya manzo nriyo yenye ploti ya vita wa Mtume Muhammad na And'aruni, mhusika nruli alowapokonya na kuwaḍ'ili waIslam katika Maḍina, Saudiya.

*82. Njia kaṭiṇḍa aḍuwa
Apitao kimuuwa
Na mali kiyatukuwa
Yao yoṭhe jazijazi.*

*83. Akiwanyang'anya mali
Yao walaḍi halali
Na wake wao ziuli
Kiwaṭaa mzimzi.*

And'aruni ananyakuwa mali, wake, na kufunga njiya za kupita misafara. WaIslam walimuwomba Mtume Muhammad awasaiḍiye kuwahifaḍi na jangili huyu ka sababu hawana menginewe wa kumliliya. Mtume Muhammad anaitikiya mito wawo na anapeleka kikosi ča maješi yake wapambane na aḍuwi huyu. WaIslam wanafyeke na kuuwawa bila huruma na jairi huyu mpaka Mtume Muhammad anašangaa vile anavowapiga maješi wake. Malaika mtukufu Jiburili anakuja na kumpaša habari kuwa huyo aḍuwi wako ana hirizi inayompa nguvu zoṭhe za kupigana hivo katika ubeti 211 /Iyu la kiṭwa ṭ'anena, Ča hoyo And'aruna, Pana hirizi baina, Yenye sifa na uyuzi/. Mtume Muhammad anamuomba Mungu amsaiḍiye kenye

vita hivo na hirizi hiyo anapokonywa huyo aduwi na anapawa yeye lakini baḍo hirizi hiyo haikumfaa Mtume Muhammad. Anamuwomba tena Allah na Mungu anamfauliṣa kumṣinra aduwi huyo na waIslam kunusurika naye.

Ploti hii taweza kusema ni ya kisiyasa ka sababu kuna viyongozi, kuna maṣitaka, kuna kuwakusanya wapiganaji panre zoṭhe mbili, kuna majamadari, na miṣo kuna miji ya kutetewa kuṭokana na uvamizi wa mṯu kuṭoka eneyo lengine. Ka hivo mand'ari yoṭhe ni ya kimapigano yenye kuhusu serikali mbili ṭafauti. Piya tufahamu kuwa mayelezo ya mand'ari haya yanatambwa kiuwazi yaani hakuna luḡa ya kiyalama au fiḥe yenye kumuwaḥa msomaji/msikilizaji kuṭokuwa kaenreleya nini kenye uṭendi. Ni kuṭokana na uwazi huu nripo tunapoṭaṭmini uwingiliyaji wa ManaLemba katika kupata sauti ya kusema yanayoṭokeya katika jamii yake ya Paṭe mnamo miyaka ya 1600. Wa Thiong'o (1994, uk. 72) anahoji kuwa fasihi ni bora zaidi kuliko historiya ka sababu fasihi huyaeleza matukiyo yoṭhe yanayoṭokeya kenye jamii ka uhalisiya halisi bila kufiḥa lolotḥe. Hii ni kuṭokana na sifa kuwa waṣairi au wanaṯi hawakujiweka kanro na siyasa (Mulokozi & Sengo, 2005, uk. 76; Ndzovu, 2014, uk. 5) na kamba uṣajiiṣaji wa kiroho (kiḍini) piya husaidiya katika kukemeya maḍila ya waṭawala juu ya waṭawaliwa (wa Thiong'o, 2016, uk. 17).

MaSufi, wanaume na wanawake, bila kubaguwa kijinsiya, wameṣiriki katika ulinganizi (Buturovic, 1996, uk. 53) ka kukemeya uḍalimu katika jamii na haswa d'uluma ya mṯu binafsi kujiḍulumu ka kumkoseya Mungu. Sifa ya muumini wa keli ni lazima aliseme la koṣa ka sababu "mIslam ni kiyoo ḥa mIslam menziwe". Kufanya hivi ni faida ka ummah na kulisemeya jambo hilo ni ka sababu ṭu ya kufunza (Knappert, 1988, uk. xiv). Tuṭawona kuwa kuṣiriki kenye siyasa kuna kuṭaṭmini hali na kisemeya juu yake haṭa kama hali ile ni ya kukuhusu wewe muumini (Ndzovu, 2014, uk. 14). ManaLemba anatupa funzo la kamba uwovu haustahmiliwi katika jamii na kusemewa juu yake

ni jukumu la kila limhusulo na ka hirizi kuṭofanya kazi mbali ya kupawa Mtume Muhammad, ni kamba suluhiṣo ni kumuwomba Mungu ka d'ati nripo utatuzi huṭokeya. Katika vita hivi Mtume Muhammad alimuwomba Mungu sana awanusuru waja wake nripo Mungu akaṁepuwa na balaa hiyo. Mtunzi anasema:

197. *Akaṭawad'a amini*
Kasali rakaṭeni
Kawinuwa ḍalihini
Uso wake muombezi.

198. *Uso wake mḥa Mungu*
Kekeza iyu la mbingu
Kamba ewe Moli wangu
Nijazi Rabi nijazi.

199. *Nijazi, nisiye ngowa*
Ewe Banangu Moliwa
Nriwe mēnye kurejewa
Al Rahimani nirizi.

200. *Ni lini ewe Ḡafaru*
Uṭakapowanusuru
Isilamu wenye nuru
Na kaumu za mṯwazi.

201. *Ka rehemayo Karimu*
Turahamusi kaumu
Urahamuwo ḍawamu
Wajao tiṣe simazi.

Mtume Muhammad alipoona wanajeṣi wake wanauawa vibaya sana alimuomba Mngu amnusuru ka sababu waumini hawana Mola mengine wa kumṭegemeya. Haṭuwa hii ya kumlekeya Mungu inaṣadiḍiya mhimili wa naḍariya yetu kuwa fasihi haiyelezi historiya ṭu bali hwitengeza historiya hiyo (Bertens, 2001, uk. 177). Kulingana na ManaLemba suluhiṣo la matatizo halimo katika juhuḍi zetu bali limo katika kumpekeṣa Mungu na kuṭaka msaada wake ṭu hivo kubaḍili mkonro wa kuṭafuṭa suluhiṣo.

Kufanya siyasa (zaidi ya kukosowa)

Katika makala haya tumependa kutafutiisha baina ya kuzungumziya siyasa na kufanya siyasa ka niya ya kulalamika lakini kupituka mipaka katika kululuma huko. Katika sehemu hii tutaangaziya namna ManaLemba alivokenra zaidi ya kulisema jambo hilo ka matumiyaji ya tamarali zenye kuwoneka kuadibiwa ni matukiyo hayo. Katika huku kuleta daaya yake nriko anakokufanya ka luha ambayo msomaji atawona mtunzi amekasiriwa mpaka anakuwa hasasi.

Wakati ManaLemba anapotongowa utendi wake na anavomsawiri nruli wake Andaruni utawona kamba kuna paradimu batini ya kitiika inayomatiri kumchora mhusika huyu. Amemita majina maovu: mlevi, nguruwe, mbwa, mtuma, setani, kafiri.

Mtunzi anamita 'mbwa' na 'mbwa mkali' kumaaniwa matusi katika ubeti 44:

44. *Hiia jabali la moshi
Lenye utiso na masi
Na hoyo mbwa kizuhi
Lake hupija zikozi.*

80. *Naye ni mbwa mkali
Andaruni juhali
Mola memolea d'uli
Motoni nriko makazi.
Kutumia neno 'kafiri' ubeti 54:*

54. *Na hoyo mbwa kafiri
Andaruni jairi
Naye asiataakhari
Mambo kitengeza kozi.
Kutumia neno 'mnwa shizi' yaani mlevi
katika ubeti 53:*

53. *Ka ubora wa husuni
Kuriifai yangani
Ikatiwa masetani
Na jamii wanwa shizi.
Pia kutumia 'nguwe (nguruwe)' katika
ubeti 146:*

146. *Na siku ya pili mewe
Katenra hiyau, nguwe*

*Walau asipumuwe
Kutaa ikawa kazi.*

Majina yote haya mtunzi ameyatumiya katika sehemu hii ya manzo kinyume na anavomsawiri nguli wake Mtume Muhammad. Halaumiki kufanya hivo ka sababu yeye nriye msanii wa kazi yake lakini katiriwa na itika za nje na kutowa luha kali kama hiyo inamfanya hisiya zake na mlemeyo wake upate nafasi ya kipaumbele na huwafiri kufanya haki ka mhusika wake. Nriposana Abou-Bakr (1992, uk. 48) anafafanua katika kazi za kifasihi kuna nafusi tatu: ya ubinadamu; ya uSufi; na ya msairi, ambapo nafusi zote hizi hujitokeza katika umoja kutokana na mapenzi alonayo msairi kama binadamu na uSufi anaotagusana nawo.

Upumbaavu wa binadamu nriyo unawomfanya ManaLemba kufanya siyasa ka kukemeya na matuwi makali ambayo hayafayi kutolewa na manachuoni kama yeye. Ni kutokana na mukadha huu nripo tunapoikiliya hoja yetu kuwa kuna itika au fikira teule yenye nguvu ya kuweza kulemaza fikira nyenginezo ili hii teule itawale. ManaLemba pengine anaamini ka kufanya fujo na kutowa maneno makali nriko kuwasiliwa malalamiwa yake didi ya hali ilivo Pate na nriko kutakompatiwa matilaba yake. Bali, siyasa yake ilikuwa ni kukemeya wanawokenra kinyume na atakayo Mola kama tutakavofafanua sehemu ijayo.

Kutumiya siyasa (kuhekimiwa na kuvunja upanga)

Luha ya kiSufi ina azma ya kumshutua msomaji ajadibike ili ilhamu imingiye apate ufahamu angalau haia kidogo shairi lasemaje (Schimmel, 1975, uk 12; Schimmel, 1982, uk 12; Hanieh, 2011, uk. 46). Zimmerman na Perkins (1995, uk. 570) na Perkins (2010) wanabainiwa kuwa kuajiliwa ni ujenzi wa fikira kimakusudi wa mthu binafsi kenye mfanyiko wa kijamii wenye shabaha ya kuleta kuhešimiyana, kuhakiki, kujali, na kuširikiwa kunrini ka wanajamii ambawo hawana mgawo manana wa maliyasili adimu ili wapate uwezo wa

kuyapata na kuyad'ibiti maliyasili hayo. Wanajamii hučukuliya kulinganiya kiđini ni katika “kazi ya kumtumikiya Mungu” na kuwafanya watu watambuwe uwezo walopawa ni Mungu (Hennink n.we, 2012, uk. 204; Lee, 2001, uk. 401).

Katika luđa ya uSufi wanaamini utukufu wa Qurani ni kuweza keleza maneno yake ka njiya zisizoidadi (Rumman, 2020, uk. 37). Ka mintarafu ya mayelezo hayo tunawajibika kusema kuwa fasiri ya *Siri* kama alivoiita mtunzi “siri ya masiri” ina maana zaidi ya moja. Na katika huku kuwa na maana nyingi tunapendekeza msimamo wetu kamba ManaLemba alitumiya siyasa ka maana ya alitumiya hekima kutowa suluhiso lake la matatizo yote kama anavoyaraitu katika utendi wenyewe: ka šida za magonjwa yoyote ubeti /509. Humepulia Manani, Na kiwee ča t'wauni, Na huma iliyo nrani, Ilo bora ya marazi;/ mašambulizi ya majini /507. Manufa'aye basiri, Nda Rihi li Ahmari, Huziwiya kula šari, Na baa za wazimzi/, na hasadi /513. Duwa hinu nabiya, Ni dawa haina šaka, Ya mačo menye kalika, Na manginge ya kuuzi;/ maajabu ya kuuwonrowa mlima /443. Ukaomba ka Jalali, Konroka kuu jabali, Katika yo majabali, Yalo bora mafumizi. 444. Lingalionroka upesi, Ka amri ya Mkasi, Na jamii ya unasi, Wakilandika maozi;/ misukosuko ya kaburini /475. Wala kabisa haoni, Zituko za kaburini, Mtu hoyo ka yakini, Ya Rabi memhifazi/, na siku ya Kiyama /477. Na Ahira ni zaidi, Hutekeleza ahadi, Na kuokoka na abadi, Na haufu na kinyezi/.

Hali kad'alika, ManaLemba anatupa suluhiso lake litokane na zile zile jazanra alizotumiya kumsawiri And'aruni kama tulizotaja—mlevi, nguruwe, mbwa, mtuma, šetani, kafiri, mjinga kama zinavoalamišwa katika uSufi. Anawašauri waumini walewe katika ulevi wa kumpata na kumjuwa Mungu; wawe watumia wa Mungu milele ka kumabuđu yeye tu (Schimmel, 1975, uk. 220); wawe kama nguruwe au Ibilisi wakubali hukumu ya Mungu alowateuwa yeye Mungu kuwa mfano wa viyumbe wengine kiga ka kufuwata amri bila kipinga—wazo lililopingwa ni maSufi wengineyo (Schimmel, 1975, kur. 195—

7). Wawe kama yule nrege meusi alompokonya And'aruni hirizi, au Maimuna farasi wa Alii [ubeti 228] kutokana na roho zawo kuwa safi hazina kinyongo wanafuwata amri. Bađili ya kumfukuza mbwa, wamaye wamfunze mpaka awe mnyama rafiki yawo. Wawe na rađa ya kumangaza Mungu katika ulimengu wote kama rađa ya makafiri wanavofiča (ka maana ya Al-Hakim, 1981) ukeli wa Mungu. Wawe šetani kama šetani wa Mtume Muhammad alosilimu na kufuwata anayoambiwa na Mtume. Wawe wayelevu wa kutambuwa miyujiza wanayopawa (hirizi aliyokuwa nayo And'aruni) ni mitego ya Mungu kujuwa wataitumiya vipi (Schimmel, 1975, uk. 212). Na kuwa mjinga kama alivokuwa Mtume Muhammad nriyo kheri kake manadamu kani moyo wake hauharibiwa na wekevu na elimu ya nje (Schimmel, 1975, uk. 218). Wawe And'aruni (viyongozi) wanyenyekevu kama anaposema yeye mtunzi “si malenga wala si mšairi” [ubeti 553] ili watu wafaidike na uwongozi wawo. Waumini wapiganiye wawe “binađamu kamilifu” na hakuna alofikia čeyo hičo ila Mtume Muhammad pekee, nriposana waIslam wote humeka Mtume Muhammad kuwa nriye kiigizo čema na kiyoo ča kujiyangaliya katika kila jambo alifanyalo katika nafusi yake (Gulen, 2011, uk. 289). Sawiya na ManaLemba anamsifu Mtume ka kumita “šarifu, mteule, mtukufu, mpenda wema, muongozi” (ubeti 162—164) zenye kuwoneša đaraja yake ka waumini.

Jazanra nyengine inayojitokeza utendini ni jazanra ya Mungu kiča “Mzamikava” ubeti wa /330. Hakika haya si winu, Asomao duwa hinu, Mzamikawa Mananu, Humjibu matongozi/. Usuli wa jina “mzamikava” ni “anayezama na kuzuka” na katika kiSwahili juwa linakotoka hwiča “kava” (mašariki) na kule linakozama hwiča “kutwa” au “zama” (mağaribi), ka hivo, Mungu anaita “juwa” katika *Siri*. Mbona Mungu aite juwa, si itakuwa ni širki ka kulijazanriša ni mungu? Juwa wazungumziyalo maSufi si juwa la mčana bali ni “juwa la usiku” haswa wa manane ambapo binađamu anakutana na

Mungu wake pekee katika giza la usiku. Na hapa juwa lineageuka kuwa nuru inayong'ara na wala si lile la mčana linaločoma (Schimmel, 1975, uk. 115). Mtume Muhammad amesema miIslamu mēnye kujizoweza kāmka usiku wa manane na kuswali Tahajjudi (swala ya usiku mkuu) basi uso wake huwa na nuru, hung'ara (Sunan Ibn Majah, Hadit' 1333). Ka hivo, ka maSufi kulala kučače usiku, kufunga sana na kunyamaa nriko kujikurubiša na Mēnyezi Mungu (Schimmel, 1975, uk. 114). Nriposana ManaLemba akahimiza waumini walipate juwa hilo la usiku ili yanyooke mambo yawo na maombi yawo yačakabaliwe maana Mtume Muhammad amesema Mungu hušuka hađi mbingu ya ard'ini wakađi wa mišo wa usiku akasikiza mačako ya kila muulizaji ayajibu.

Matumiyaji ya țarakimu na abjađi za kiArabu katika kazi za kiSufi ni katika siri k^huu nyenginezeo ambazo kumefičamana mambo ambayo waliyomo Sufini nriyo wenye kuyajuwa. Kila herufi ya abjađi ya kiArabu imepawa hesabu yake na inaaminika ka kufuwata hesabu hizo basi matenro ya m^hu huweza kučabirika au kutatuka ikiwa ana šiđa (Schimmel, 1975, uk. 412; wa Mutiso, 2014). Elimu hii hwița elimu ya falaki na maSufi wamekuja kitumiya katika maiša yawo hața katika mambo ya kumsaiđiya manamke anapokuwa na šiđa ya mazazi (Al-Ghazali, 1952, uk. 80) na ni mjarabu. Hali kađ'alika katika *Siri* mtunzi ametumiya țarakimu hizi, pengine kisađifa, kama abainišavo Rumman (2020, kur. 54-55) wasimamizi wa țariqa za uSufi wamepangika: 2 (kama Mtume Muhammad na Ali bin Abi Talib makamanra wa ješi [ubeti 185]), 4 (kama makhalifa wa uwIslamu Abubakar, Umari, At'mani, Ali [ubeti 13-14]), 7 (kama safu za wanaješi [ubeti 352]), 10 (kama walobaširiwa pepo na Mtume Muhammad waloađamana naye kēnye vita na And'aruni [ubeti wa 88-99]); 12 kama miyezi katika maka na hesabu hii henra mpaka 99 ambayo ni majina mačukufu ya Mungu (ubeti 531). Piya tujuwe kuwa uťeđi huu unaiša ka wiťiri (hisabu isogawika nusu ka nusu lazima iťabaki 1) yaani iđađi ya beti ni 563. Ka maSufi wiťiri ni kušađiđiya

maneno ya kiyelelezo čawo Mtume Muhammad kamba Mungu ni wiťiri anapeđa mambo wiťiri, na zaiđi, ni kuregeleya sifa yawo k^huu ya upekee (umosi) wa Mungu. Matumiyaji ya țarakimu hivo ka maSufi si kisađifa bali kuna elimu yake na ka elimu alonayo ManaLemba yaweza kuwa aliitumiya kițamaťali katika uťeđi.

Sifa k^huu ya maSufi ni kučawakali yaani kumťegemeya Mungu pekee katika mambo yoťhe ya kimaiša ya kiđuniya na kiyahera ili kusitokee čembe ya fikira kamba m^hu fulani aweza kumsaiđiya katika jambo lake (Schimmel, 1975, uk. 117) yaani wamekinayi (Bang, 2003, uk. 20) na alivopanga Mungu. MaSufi humťegemeya Mungu sana mpaka kuna wengine hufasiri kivingine kamba uSufi huwenreleza uvivu au huvunja moyo wa kusifanywe kazi au kusifanywe juhudi yoyoťhe ya kujiyenreleza kimaiša (Gulen, 2011). Taswira hii ya kumťegemeya Mungu ka kila k^hit^hu haimaniši kuwa uSufi haumo kēnye maiša (Rumman, 2020, uk. 350) bali ni ile imani yawo kuwa kila anayemťii Mungu ka ukamilifu woťhe basi kila kiličoumbwa načo humťii yeye Sufi (Schimmel, 1975, uk. 207). Nriwo alivofanya mtunzi kuanza kutunga uťeđi wake ka kuwomba msaada kučoka ka Mungu na ubeti 563, mišo wa uťeđi, anamaliziya ka kauli țukufu ya “hapana Mola wa kabuđiwa ila Allah pekee”. Imam Al-Ghazali (1952, uk. 152) amefafanuwa kučawakali ka Mungu ka maana ya mja akitumiya đini kama njiya ya kujinufaiša katika ulimengu huu (kama And'aruni) basi aťahasirika đuniya zoťhe mbili—ya hapa na ya ahera. Na m^hu mēnye kuwața ulimengu huu ka ajili ya Mungu basi aťafaiđika đuniya zoťhe mbili—ya hapa na ya ahera (kama Mtume Muhammad). Ka imani hii basi maSufi wanastahabu wawe mafakiri milele ka Mungu Mpaji humu đuniyani ili waipate đuniya hii waliyomo na hiyo pepo; na kupata kawo si kupata vit^hu bali ni kupata rad'i na rehema za Mungu (Rumman, 2020, uk. 43) ambazo nrizo šabaha ya kila Sufi. Huku kurid'iwa na Mungu nriko kutumiya siyasa ManaLemba kuwawoneša wasomaji na wanađamu woťhe kuwa kuťegemeya Mungu tu

katika majambo yote nriko kuletako masuluhisho ka kila matatizo ilimrahi imani yakinifu. Alipoširwa vitani Mtume Muhammad aliyomba /319. Ya Rabbi anta arhamu Fa ma lahum Maula Ġairuka ya Rabbi/ (Ewe Mola wewe nriwe mrehemewu hawana Mola menginewe isipokuwa wewe). Piya, kinga na ngome ya kutegemewa katika jambo lolote ni Mungu tu anapomaliziya utendi wake ka /563. La Ilaha ila llahu, La Ilaha ila llahu, La Ilaha ila llahu, Peke Mola Muawazi/. (Hapana Mola wa kabudiwa ila Allah x3 Peke yake nriye Mlipaji). Mlamali (1980, uk. 6) anayeza kuwa “La Ilaha ila llahu” ni ngome ya Allah na menye kingiya husalimika. Zaidi, Gulen (2011, uk. xxviii) anatambuliša kuwa maSufi hutafuta kufahamu maana ya “la haula wala kuwata illa billah” yaani “Hapana uwezo wa kufanya wema wala nguvu ya kutofanya ubaya illa ka idini ya Allah” sawiya ManaLemba ubeti wa 208 & 326. Ketu sisi yaonekana Mungu nriye “nguvu kuu na pekee” katika maiša ya manadamu na haya ya nguvu kuu iliyotawaliwa na kuhalaliwa ni wanahi nriyo yahiitajiwayo katika kenreša mambo ya kiserikali na kimiji (Heywood, 2013, uk. 4). Na piya Allah anamambiya mtumewe, “hukutupa [mafumo] ulipotupa, lakini ni Allah aloṭupa” (Al Anfaal:17) ili ijulikane Yeye nriye mtenra mambo (Gulen (2011, uk. 294). Nriposana tukasema kauli ya mišo ya ManaLemba anahekimiša waumini watumiye kauli hiyo ka kila jambo hata wanapohujumiwa kisiyasa.

HIṬIMIŠO

Makala haya yamejaribu kufafanua maana za neno siyasa kenye matumiyaji yake kinahau. Tumepata kuwa kuna siyasa ambalo ka mayelezo ya tasnia yake hujumiša kupelekeša mambo katika jamii au serikali. Kuna sosiyasa isojišuguliša ni siyasa kabisa, ikiwa yawezekana, kutokana na mafundisho ya kifamiliya au uwamuzi wa mthu mnyewe. Utafiti wetu wa nahau za kiSwahili umepambanua kuwa kuna maana tafauti wakati neno siyasa linapošikaniwa na neno lengine na hivo ipo haja ya kangaliya miktaḍa tafauti ya matumiyaji hayo. Nahau kusikiya siyasa, kingiliya

siyasa, kufanya siyasa na kutumiya siyasa zina maana ya kuhisi matukiyo ya kisiyasa, kujitosa kenye ulingo wa siyasa, na kutumiya hekima wakati wa mašauriano yoyote ya kijamii kimtawaliya. Kutokana na maana hizi zetu tuliweza kučanganuwa matini ya *Uṭendi wa Siri li Asrari* uliyotungwa ni Manamarabu binti BanaLemba mnamo 1662 BK. Katika mfanyiko huu wa uanganuzi tuliweza kuširikiša ḍana za siyasa, uSufi, na ušajiišaji unavoweza kupa utendi fasiri mpya tafauti na walivofanya watafiti walotutanguliya. Siyasa huhusiyana na ušajiišaji na ušajiišaji hutokeza ka sababu ya tafauti za maslahi ya kijamii na dini. Kisisi, uSufi, nriyo itikaḍi iliyotawala miyelekeyo ya mtunzi. Mkusanyiko wa mambo yote haya yanawafiki naḍariya ya uHistoriya Mpya tulotumiya yenye msimamo kuwa matini ya kifasihi šaruti iweke kenye muktaḍa wa kihistoriya wakati na mahali ilipokuwa yasanifiwa. Haya ni ka faida ya kuzuwa mambo ambayo hayakelezwa ni msanii lakini yanajitokeza muktaḍa huwo unapotiliwa maanani na katiri fasiri za kazi hiyo.

Šukurani

Tamtabarukiya makala haya Marehemu Profesa Abdallah S. Bujra, mmoja wa waanziliši wa CODESRIA. Alifariki juzi ilhali tumo kenye kuyakamiliša makala haya na kisaḍifa tulikuwa tumenukuu kazi yake. Allah amtangamaniše na wema peponi, Amiin.

MAREJELEO

- Abou-Bakr, O. (1992). The symbolic function of metaphor in medieval Sufi poetry: The case of Shushtari. *Alif: Journal of Comparative Poetics* 12, 40-57. <https://www.jstor.org/stable/521635>
- Bang, A. K. (2003). *Sufis and scholars of the sea: Family networks in east Africa, 1860-1925*. RoutledgeCurzon.
- Al-Beidh, M. S. S. (2011). *Tarehe ya east Africa*.pdf

- Bertens, H. (2001). *Literary theory: The basics*. Routledge.
- Biersteker, A. (1991). Language poetry and power: A consideration of “Utendi wa Mwanakupona”. Katika K. W. Harrow (mh.) *Faces of Islam in African literature*, 59—78. Heinemann Educational Books.
- Boxer, C. R. and Azevedo, C. (1960). *Fort Jesus and the Portuguese in Mombasa*. Hollis and Carter.
- Bujra, A. S. (2017). Conclusion: Research issues concerning Hadhramaut. Katika N. Brehony (mh.), *Hadhramaut and its diaspora Yemeni politics, identity and migration*, kur. 225—232. I. B. Tauris.
- Buturovic, A. (1996). Spiritual empowerment through spiritual submission Sufi women and their quest for God. *Canadian Women Studies*, 17 (1), 53—56.
- Dammann, P. E. (1940). *Dichtungen in der Lamu mundart des Suaheli Band 28*. Freiderichsen.
- Al-Ghazali, H. (1952). *Deliverance from error and attachment to the Lord of Might and Majesty*. Imetafsiriwa na Montgomery Watt. George Allen and Unwin Ltd.
- Gulen, M. F. (2011). *Emerald hills of the heart: Key concepts in the practice of Sufism 2*. Tughra Books.
- Al-Hakim, S. (1981). *Mu'jam AlSufi* (Sufi Lexicon) (1st ed.). Dar Nadrah for Printing and Publishing.
- Hanieh, H. (2011). *Sufism and Sufi orders: God's spiritual paths adaptation and renewal in the context of modernization*. Friedrich-Ebert-Stiftung.
- Hennink, M., Kiiti, N., Pillinger, M & Jayakaran, R. (2012). Defining empowerment: Perspectives from international development organisations. *Development in Practice* 22 (2), 202—215. <http://dx.doi.org/10.1080/09614524.2012.640987>
- Heywood, A. (2013). *Politics* (4th ed.). Palgrave Macmillan.
- Karama, M. (2018). *Maana timilifu kutokana na undimi katika utendi wa siri li asrari*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), Pwani University, Kilifi.
- Karama, M., Chimera, R., na wa Mutiso, K. (2018). Ushairi wa kiSufi katika tendi za kale za Kiswahili: Mfano wa utendi wa siri li asrari. *Mara res. j. Kiswahili* 3 (1), 1 – 9.
- Karama, M., Chimera, R. & Kineene, M. (2021). Si tendi za kabla ya karne ya ishirini ni utambaji wa kingano nyengine ni ufunzaji: Kiyelelezo cha utendi wa siri li asrari. *East African Journal of Swahili Studies*, 3(1), 51-57. <https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.349>.
- Knappert, J. (1979). *Myths and legends of the Swahili*. East African Educational Publishers.
- Knappert, J. (1988). *Four centuries of Swahili verse: A literary history and anthology*. Darf Publishers Limited.
- Lee, J. A. B. (2001). *The empowerment approach to social work practice building the beloved community* (2nd ed.). Columbia University Press.
- Madan, A. C. (1903). *Swahili - English dictionary*. Clarendon Press.
- Martin, C. M. P. & Martin, E. B. (1973). *Quest for the past: An historical guide to the Lamu archipelago*. Marketing and Publishing Limited.
- Mlamali, M. (1980). *Al Inkishafi: Ikisiri ya Mlamali*. Longman Kenya.

- Muhammad, Y. K. (2003). *Almausuatu alyusufiyah fi bayani adillah alSufiyah* (The Yusufiya encyclopedia in explaining the evidence of Sufism). Daru Taqwa.
- Mulokozi, M. M. & Sengo, T. S. Y. (2005). *History of Kiswahili poetry A.D. 1000 - 2000*. Institute of Kiswahili Research.
- Mustafa, I. (2004). *Mu'jam Al Wasit* (Intermediate dictionary) (4th ed). Al-Shorouk National Library.
- Wa Mutiso, K. (2003). *Utenzi wa siri li asirali [afuan] with a translation in English*. Mswada haujachapishwa. Kanzi ya Profesa Kineene wa Mutiso.
- Wa Mutiso, K. (2014). Number symbolism in world religions: The case of number seven. *Journal of Oriental and African Studies*, 23, 405-415.
- Ndzovu, H. J. (2014). *Muslims in Kenyan politics political involvement, marginalization, and minority status*. Northwestern University Press.
- Perkins, D. D. & Zimmerman, M. A. (1995). Empowerment theory, research, and application. *American Journal of Community Psychology* 23 (5), 569—579.
- Perkins, D. D. (2010). Empowerment. Katika R.A. Couto (mh.), *Political and civic leadership: A reference handbook*, kur. 207-218. Thousand Oaks.
- Rom, M. C., Hidaka, M. & Walker, R. B. (2022). *Introduction to political science*. OpenStax.
- Roskin, M. G., Cord, R. L., Medeiros, J. A., Jones, W. S. (2012). *Political science: An introduction* (12th ed.). Longman.
- Rumman, M. (2020). *Mysteries of the Sufi path: The Sufi community in Jordan and its zawiyas, hadras and orders*. Friedrich-Ebert-Stiftung.
- Sameja, M.A. (h.t.). *Aali Ba Alawiy: Sehemu ya kwanza.pdf*
- Schimmel, A. (1975). *Mystical dimensions of Islam*. The University of North Carolina Press.
- Schimmel, A. (1982). *As through a veil: Mystical poetry in Islam*. Columbia University Press.
- Sell, T.M. (2023). *An introduction to politics*. Libretexts.
- Shariff, I. N. (1988). *Tungo zetu: Msingi wa mashairi na tungo nyenginezo*. The Red Sea Press.
- Sheriff, A. (2002). *Slaves, spices, & ivory in Zanzibar: Integration of an east African commercial empire into the world economy, 1770-1873*. East African Educational Publishers.
- Wa Thiong'o, N. (1994). *Writers in politics: Essays*. East African Educational Publishers.
- Wa Thiong'o, N. (2016). Abdilatif Abdalla and the voice of prophecy. Katika R. M. Beck & K. Kresse (wah.), *Abdilatif Abdalla: Poet in politics*. Mkuki na Nyota Publishers Limited. 11—18.
- Tindall, W. Y. (1955). *The literary symbol*. Columbia University Press.
- Van Deth, J. W. (2021). What Is Political Participation? DOI:10.1093/acrefore/9780190228637.013.68
- Walker, I. (2017). Citizenship and belonging among the Hadhramis of Kenya. Katika N. Brehony (mh.), *Hadhramaut and its diaspora Yemeni politics, identity and migration*, kur. 164—182. I. B. Tauris.
- Wikipedia.org.
https://en.m.wikipedia.org/wiki/George_Eliot

Wilde, D. (h.t.). On Sufism and Poetry.
<http://www.unc.edu/depts/Sufilit/Wilde.html>